



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA



Tarehe: 18 Aprili, 2023

TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI TAREHE
27 – 30 APRILI, 2023

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma kupitia kibali cha Ajira cha tarehe 09 Februari, 2022 chenye Kumb. Na. FA. 170/360/01"A"/56, anapenda kuwatangaiza waombaji wote walioomba nafasi za kazi kwa mujibu wa Tangazo lenye Kumb. Na. HMD/S.20/39/38 ya tarehe 9 Machi, 2023 kuwa, usaili kwa walioomba nafasi ya Mwandishi Mwendesha Ofisi Daraja la II na Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II utafanyika katika Ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuanzia saa 2:00 asubuhi kwa Mchanganuo wa Ratiba kama ifuatavyo:

Na.	Kada	Tarehe ya usaili wa mchujo	Tarehe ya usaili wa vitendo	Tarehe ya usaili wa mahojiano ya ana kwa ana
1.	Mwandishi Mwendesha Ofisi II	Hakuna	27 Aprili, 2023	28 Aprili, 2023
2.	Msaidizi wa Kumbukumbu II	29 Aprili, 2023	Hakuna	30 Aprili, 2023

Waombaji wote walioitwa mnaelekezwa kufika na vyeti vyenu halisi, pamoja na mojawapo ya vitambulisho vifuatavyo, (kitambulisho cha NIDA, kitambulisho cha Mpiga kura, kitambulisho cha Mkazi, Hati ya kusafiria, leseni ya udereva na barua ya utambulisho kutoka Serikali ya Mtaa).

Kwa wale ambao hawakuona majina yao ifahamike kuwa hawakufanikiwa kupata nafasi ya kuitwa kwenye usaili, hivyo waombe tena nafasi wakati mwingine.


1 Mtaa wa CDA, S.L.P. 1249, 40477 Dodoma, Tanzania. Simu: +255 (026) 234917,
Nukushi: +255 (026)-23211550, Barua Pepe: cd@dodomacc.go.tz, Tovuti: <http://www.dodomacc.go.tz>

Aidha, orodha ya majina ya walioitwa kwenye usaili imeambatishwa.

Nawatakia kila la kheri.



Joseph C. Mafuru
MKURUGENZI WA JIJI
DODOMA



1 Mtaa wa CDA, S.L.P. 1249, 40477 Dodoma, Tanzania. Simu: +255 (026) 234917,
Nukushi: +255 (026)-23211550, Barua Pepe: cd@dodomacc.go.tz, Tovuti: <http://www.dodomacc.go.tz>